



TANGAZO LA KAZI KWA NAFASI YA FUNDI RANGI (Maalumu kwa vyuma)

BESIX Ballast Nedam (BBN) Limited, ni MKANDARASI anayehusika na uhandisi, ununuzi na ujenzi wa gati na kituo cha kupakia mafuta ghafi ya mradi wa EACOP, anakaribisha maombi kwa nafasi ya kazi ya Fundi Rangi (Maalumu kwa vyuma).

| | |
|------------------|--------------------------------------|
| Mradi | EACOP – Jetty & Loading Out Facility |
| Muajiri | BESIX Ballast Nedam Limited (BBN) |
| Mahali pakazi | Tanga |
| Nafasi ya kazi | Fundi Rangi (Maalumu kwa vyuma) |
| Mkuu wa Idara: | Meneja Ujenzi |
| Kipindi cha kazi | December 2023 – May 2025 |

Dhumuni la kazi

Fundi rangi atakua na jukumu la kupaka rangi kwa kiwango cha hali ya juu katika vyuma na vifaa vingine ambavyo vinatumika katika sekta ya mafuta na gesi. Fudi rangi atapaka rangi katika maeneo na mazingira tofauti tofauti kwakutumia mashine za kisasa za kupuliza rangi.

Majukumu ya kazi

- Kutunza vifaa vya kazi.
- Kuandaa eneo la kupulizia rangi kwa kutumia maji kusafisha, kuparaza kwa mashine na/au kwa njia nyinginezo.
- Kuandaa mashine ya kupulizia rangi.
- Kupulizia rangi kwa kutumia njia tofauti tofauti kama vile Manuel na Vacuum.
- Kuhakikisha rangi yote inapulizwa au kupakwa kwa kuzingatia viwango husika vya sekta na pia kanuni mbalimbali kama vile NACE na SSPC.
- Kuwa na ujuzi wa kutosha na pia uthibitisho toka kwa taasisi maalumu za rangi kama vile AMPP, NACE na FROSIO.
- Kutunza vyema kumbukumbu za kazi iliyofanyika na pia vifaa viliviyotumika.
- Kuwasiliana na wafanyakazi wenzako na pia viongozi wako ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi.

Sifa za muombaji.

Muombaji awe na sifa zifuatazo:

- Awe raia wa Tanzania
- Elimu ya Diploma au taaluma nyingine yeoyote husika kwa kazi hii.
- Vyeti vya mafunzo muhimu kwa kazi ya rangi



EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE



- Angalau uzoefu usiopungua miezi mitatu kwa kazi ya rangi hasa katika sekta ya mafuta na gesi.
- Ufahamu wakutosha kuhusu viwango stahiki katika sekta ya rangi kama vile NACE na SSPC.
- Uwezo wa kusoma na kuelewa michoro na maelekezo ya kitaalamu.
- Uzoefu wa kutumia vifaa na namna tofauti tofauti za kupaka rangi kama vile Manuel na Vacuum.
- Umahiri na umakini wa kuzingatia maelekezo na viwango vya ubora.
- Uwezo wa kufanya kazi kwa kushirikiana.
- Uwezo wa kufanya kazi katika hali zote na pia maeneo ya ndani na ya nje.
- Utayari wa kufanya kazi muda tofauti tofauti ikiwa ni pamoja na usiku au siku za mwisho wa wiki pale inapohitajika.

Jinsi ya kutuma maombi:

Maombi yote yatapokelewa kupitia email address jobs@bbnltd.co.tz na mwisho wa kupokea maombi haya ni 19 Octoba 2023.

HAKUNA AJIRA MLANGONI!!! USITOE HELA KUPATA KAZI!!!

TAMBUA KUWA, endapo hatutawasiliana na wewe wiki mbili baada ya tarehe ya mwisho ya tangazo hili, maombi yako yatakuwa hayajafanikiwa.